Kuishindania Imani Kikamilifu

na

Ellis P. Forsman

Kuishindania Imani Kikamilifu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Kuishindania Imani Kikamilifu

Yuda 1:3-4

Tunapoanza kutazama katika kusudi la Waraka Wa Yuda, tunaona kwamba shauku yake halisi ilikuwa ni kuandika kuhusu wokovu wetu imara tulioshiriki pamoja na Kristo: Yuda 1:3, "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*"

Hitaji la kubadilisha kusudi lake tunaiona katika mustari unaofuata: Yuda 1:4, "*Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliyepeke yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Kwamba watu "*wamejiingiza pasipo kujijua"* lazima tuvute pumzi kwanza. Kwamba hiyo inaweza kutokea, bila kujali maonyo mengi yaliyotolewa na Yesu, Paulo, na Petro. Ni rahisi kiasi gain, basi, kwa hili kutokea leo tunapoishi katika nyakati zilizowekwa mbali na maonyo hayo! Kuhusu swala hili, Yuda anawasii watu "*Waishindanie imani kikamilifu"* inakuwa wazi hata kwetu sisi leo hii.

Tunapaswa kushukuru "*hitaji*" la kuishindania imani. Tunapaswa kuelewa "*ni jinsi gain*" inapofika wakati wa kuishindania imani kikamilifu.

Katika somo hili, "Kuishindania Imani Kikamilifu", ni "hitaji" na "jinsi gani" tunapoitazama kwa ukaribu zaidi.

"Hitaji" la kuishindania imani kikamili

Baadhi watakataa ubora wote wa maandiko. Hii inaweza kutazamwa kutoka katika neno "*imani iliyotolewa mara moja kwa watakatifu.*" Msisitizo "*mara moja kwa yote*" kwa usahihi inaweza kunyumbulishwa "mara moja kwa wakati wote". Hiyo nii "*imani*" (fundisho hilo lote ambalo tunapaswa kuliamini) lilitolewa kwa kanisa "wakati mmoja kwa nyakati zote".

Ufunuo haikupaswa kurudiwa, na hakukua na cha zaidi ili iweze kufunuliwa baadaye! Kwamba Mungu amefunua yote haya ambayo anatutaka sisi kuyajua kwa udhibitisho kutokana na kauli kama ya:

Paulo, akiwambia wazee wa Efeso: Matendo. 20:27, "*Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiri ya kusudi lote la Mungu.*"

Tuna "*vitu vyote*", na kama tuna mausia yote ya Mungu", kuna nini kingine? Hivyo maandiko, yaliyo na imani iliyotolewa "*mara moja kwa yote*", yana kila kitu tunachokiitaji ili tuwe kile ambacho Mungu anatutaka tuwe! 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Lakini watu wanapopendekeza kwamba ufunuo wa Mungu haujakamilika, au bado ipo katika muendelezo; au kwamba ufunuo wa Mungu unahitaji kurudiwa; basi kazi yetu ni "*kuishindania imani iliyotolewa mara moja kikamilifu*"!

Baadhi watapotosha mafundisho ya neema.

Kulikuwa na watu wakati wa Yuda "*waliogeuza neema ya Mungu kuwa katika uchafu* (ufisadi)". Mafundisho yao ya neema yaliwapa udhuru wa kutenda dhambi. Hivyo zaidi sana, wakajiingiza katika kile ambacho kilikuwa ni aibu ya wazi (uchafu). Labda walisema kama katika Waru. 6:1, "*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?*

Kuna wengine leo wanaopotosha neema ya Mungu kwa kutoa udhuru wa kutokuzingatia amri zinazopatikana katika Neno la Mungu; kuthibitisha mfumo wa maisha yao kwamba iko kinyume na mifumo ya Biblia. Kwa sababu wanaweza wakasema: "Mungu ana upendo mwingi – neema yake ni ya ajabu – kutuhukumu tunapokuwa wema!"

Bali wale wanao "*shindania imani kikamilifu*" watakumbushwa mara zote hakika juu ya kile neema ya Mungu inayofundisha. Tito 2: 11-12, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote, imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tama za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, mkatika ulimwengu huu wa sasa;*"

Neema ya Mungu utufundisha kukataa vitu visivyo vya kiungu na tama za dunia! Inatufundisha kuishi kwa utaratibu, haki, na uungu katika wakati huu uliopo.

Wengine watakataa mamlaka ya Mungu.

Yuda alishughulikia wale ambao "*…wanamkana Bwana Mungu pakee na Bwana Yesu Kristo*".

Msisitizo unatokea katika neno "Bwana", ilivyotumika kuelezea Mungu na Yesu. Neno "bwana" inatokana na neno kurios {koo'-ree-os}, ambayo inahusishwa na neno kuros (ukuu); ikimaanisha "ukuu katika mamlaka".

Watu hawa walikuwa wakikataa mamlaka sahihi ya Mungu na Yesu.

Leo mara nyingi tunakutana na watu wakikataa mamlaka ya Mungu na Yesu kwa utovu wao wa nidhamu kwa Neno La Mungu; kwa kuweka misingi yao wenyewe ya mamlaka kwa kile wanachokiamini na kukifanya; kama vile watu maarufu, karamu, sehemu ya kufikia; kama vile papa, shemasi, wahudumu, au watu wao wenyewe.

Bali wale "*wanaoishindania imani iliyotolewa mara moja kikamilifu*" wata tambua mamlaka ambayo ni ya Kristo.

- Math. 28:18, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*"
- Efe. 1:21-22, "*Katika yeye jengo lote linaungamanishwa na kukua hata liwe hekalu takatifu la Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mmejengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*"
- Yoh. 13:20, "*Amin, amin, nawaambieni, yeye ampokeaye mtu ye yote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi; ampokea yeye aliyenipeleka.*"
- 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"
- 1 Wathes. 2:13, "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo ilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.*"
- Matendo. 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*"

Wazi wazi hitaji la "*kuishindania imani kikamilifu*" ipo, kama jinsi kulivyokuwa na wale nyakati za Yuda waliokataa ukweli wote wa neno la Mungu, wakapotosha mafundisho ya neema, na kukataa mamlaka ya Mungu na Yesu; hata sasa kuna watu kama hao leo hii! Sasa tutaifanyaje?

"Jinsi gani" kuishindania imani kikamilifu

Lazima tushindane kikamilifu. Swala hili lina maanani; tupo vitani! Paulo anaelezea uasilia wa vita vyetu:

- 2 Kor. 10:3-6, "*Maana ingawa tunaenda katika mwili, hatufanyi vitu ya jinsi ya mwili; maana silaha ya vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha*

mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwenu kutakapotimia."

- Efe. 6:10-13, "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kuzipinga hila za shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama.*"

Huu sio wakati wa kutokuwa tayari; lazima tuvae silaha! Hivyo basi lazima tushindane kwa shauku, hata kufikia hatua ya kifo, kwa "*imani iliyotolewa mara moja kwa watakatifu*"!

Lazima tutumie silaha katika kujikinga kwetu. Paulo anafafanua silaha zetu katika Efe. 6:13-18, "*Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani, ; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.*"

- Kujifunga na kweli.
- Ngao ya haki.
- Miguu imefungwa kwa injili ya amani.
- Chepeo ya wokovu
- Kuvaa dirii ya haki kifuani.
- Upanga wa Roho, Neno la Mungu.
- Kwa sala zote na maombi.

Kumbuka kwamba wingi wa vitu hivi ni kwa ajili ya kujikinga kwetu, tusije tukapotea katika jitihada! Chembechembe ya kweli, haki, injili, imani, wokovu, n.k., vinahitajika kwa ajili ya wokovu wetu wenyewe zaidi na kwa wale tunaowatafuta kuwashinda.

Wengi wanakua haraka katika kuchukua chepeo, wakiacha silaha zingine!

Paulo pia alikuwa na kitu cha kusema kuhusu silaha zingine ambazo ni "ukuu katika Mungu". Ubora kama huu unapatikana katika: 2 Kor. 10:1-6, "*Basi mimi Paulo mwenyewe nawasihi kwa upole na utaratibu wa Kristo, mimi niliyemnyenyekevu nikiwapo pamoja nanyi, bali nisipokuwapo ni mwenye ujasiri kwenu; naam, naomba kwamba nikiwapo, nisiwe na ujasiri kwa uthabiti ambao nahesabu kuwa nao juu ya wale wanaodhania ya kuwa sisi tunaenda kwa njia ya mwili. Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwenu kutakapotimia.*"

Kuhakikisha kwamba sisi ni wa kwanza "kiroho", na pia kuonyesha upole na tahadhari. Wagal. 6:1, "*Paulo mtume, si mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali na Yesu Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka katika wafu.*"

Tukiachana na mapigano, na kuweka upole. Neno, pamoja na ukarimu na uungwana unarekebisha upande. 2 Tim. 2:23-26, "*Walakini uyakatae maswali ya upumbavu yasiyo na elimu, ukijua ya kuwa huzaa magomvi. Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua kweli;wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa ibilisi, ambao hao wametegwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake.* "

Hitimisho

Wito wa "*kuishindania imani kikamilifu*" haijawa kimya kuweza kuleta "mfarakano" na "kupasuka kwa hasira".

- Wagal. 5:19-21, "*Basi matendo ya mwili ni dhahiri ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo, hawataurithi ufalme wa Mungu.*"

- 1 Kor. 3:1-3, "*Lakini ndugu zangu mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula, kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna*

husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?"

Bali ni wito wa kushindana kwa silaha zote zilizoko upande wetu. Kwanza awali ya yote, kwa neno la Mungu, litumike kwanza kwetu sisi na baadaye kwa wengine. Lakini pia, na ubora unaofanana na wa Kristo ambayo yana "ukuu katika Mungu" kuwaleta watu wamtii Kristo.

Katika hili ukweli kwamba wengi hawamtii Kristo na Bwana, bali wanapotosha mafundisho yake au kujiweka wenyewe juu kama mamlaka yao wenyewe. Hiyo inaifanya iwe muhimu kwamba "*tuishindanie imani iliyotolewa mara moja kwa watakatifu wote".*

Katika vita hivi WEWE uko upande gain? Je umejitoa kwake yeye ambaye Mungu amemfanya kuwa Bwana na Kristo? Je unaendelea kusimama katika fundisho la mitume?

Matendo. 2:36-42, "*Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo. Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na Mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana, na kuwaonya akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. Wakawa wakidumu katika fundisho la Mitume, na katika ushirika na kkatika kuumega mkate, na katika kusali.*"